

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA AFYA

### MKOA WA NJOMBE

Anuani "Afya"

Nambari ya Simu +25526-2782912

Nukushi: +225-26-2782914

Baruapepe: [njomberrh@afya.go.tz](mailto:njomberrh@afya.go.tz)

Tovuti: [www.njomberrh.go.tz](http://www.njomberrh.go.tz)



Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,  
14 Br. Ya Hospitali ya Rufaa,  
59107 Ramadhani-Njombe,  
S.L.P 1044,  
**NJOMBE**

## HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA NJOMBE

### KITENGO CHA MAWASILIANO NA UHUSIANO

#### TANGAZO LA AJIRA YA MKATABA

Kuh: NAFASI YA AFISA HABARI MSAIDIZI DARAJA LA I -TGS C

**Septemba 04, 2023**

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Njombe, anawaalika Watanzania wenye sifa za kuomba nafasi ya kazi ya mkataba katika nafasi Afisa Habari.

Hivyo Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe anawatangazia Watalaam wa kada ya Afisa Habari wenye sifa, kuwasilisha barua ya maombi ikiambatishwa na wasifu (Curriculum Vitae) kwa ajili ya kuomba nafasi ya kuwa Afisa Habari wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe.

#### SIFA ZA MUOMBAJI

- Awe amehitimu kidato cha nne au cha sita mwenye Stashahada ya Habari kutoka Vyuho vinavyotambuliwa na Serikali na mwenye uzoefu wa kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja katika fani ya habari.
- Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta

#### KAZI NA MAJUKUMU


- i. kutafiti na kuandika habari
- ii. kusimamia Maktaba ya picha na Maktaba ya Marejeo
- iii. Kupokea maoni/hoja za wananchi na kuziwasilisha sehemu husika
- iv. Kuandaa majarida, mabango na vipeperushi vinavyohusu shughuli za maendeleo ya sehemu husika.
- v. Kupiga picha za mnato
- vi. Kupiga picha za video

## NAMNA YA KUWASILISHA MAOMBI

Muda wa kutuma maombi haya ni ndani ya wiki mbili (2) tangu tarehe ya kutoka kwa Tangazo hili. Aidha, mwisho wa kupokea maombi ni Septemba 17,2023 saa 5:59 Usiku.

Muombaji unapojibu tafadhali taja:

Mganga Mfawidhi,  
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,  
S.L.P 1044,  
**NJOMBE.**



Hassan Majaliwa

Kny:- Afisa Mawasiliano Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Njombe.